

Mafundisho ya Biblia

Imeandikwa Ministries

# PAMBANO KUU

Mch. Almodad Amos

Release 01 @ 2021

# Asomaye na Afahamu

**Haiwezekani Kufahamu, Mpaka Kwanza Umesoma au umesikia kutoka kwa aliyesoma Neno la Bwana**

Mathayo 24:15; Warumi 10:17

Haki zote zimehifadhiwa. Unaruhusiwa kusambaza kwa njia ya kidijitali lakini sio kuuza kwa namna yoyote ile bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa kitabu hiki. Ukihitaji nakala iliyochapishwa wasiliana na mwandishi kwa
+255718834621 | modaofpeace@gmail.com

# PAMBANO KUU

## MUHTASARI

Hili ni somo moja miongoni mwa masomo Manne yanayoangukia katika kundi la Mafundisho ya Biblia linaloitwa Fundisho Kuhusu Wokovu. Somo hili linaitwa Pambano Kuu, ambalo ni Imani ya Msingi No. 8 miongoni mwa Imani za Msingi 28 kama zinavyofundishwa na Kanisa la Waadventista wa Sabato. Baadhi ya mambo tutakayoangazia katika somo hili li pamoja na:

- Maana ya Pambano Kuu
- Eneo pambano hili linapofanyikia
- Mwasisi wa pambano hili
- Wahusika wakuu wa pambano hili
- Mbinu zinazotumika katika Pambano
- Na hatimaye mpango wa Mungu katika Pambano Hili.

## UTANGULIZI

Huhitaji kuchagua ili uingie ndani ya hili pambano. Tayari wote tumeshahusishwa. Na hata maisha ambayo tunaishi yamekaa mkao wa Pambano: Kuna mbele na nyuma, kuna kulia na kushoto, kuna kupata na kupoteza, kuna furaha na huzuni, n.k. Ukiichunguza Biblia kwa umakini utaona sura mbili zinazojitokeza toka mwanzo wa Biblia mpaka mwisho wake: Angalia mifano hii michache:

- Kuna kweli na uongo
- Kuna watoto wa Mungu na kuna watoto wa Ibilisi
- Kuna uzima wa milele na kuna mauti ya milele
- Kuna upande wa nuru na kuna upande wa giza
- Kuna mlango mwembamba na kuna lango pana
- Kuna njia nyembamba na kuna njia pana
- Kuna mpanzi wa mbegu njema na mpanzi wa magugu
- Kuna kundi la kondoo na kunzi la mbuzi

## MWONEKANO WA ATHARI ZA PAMBANO

Wanadamu wengi wameelekeza fikra zao katika kutafuta chanzo na sababu hasa ya kuwepo kwa pande hizi mbili ambazo zimezaa taabu na mahangaiko makubwa katika ulimwengu huu. Mwisho wa tafiti zote huwa wanadamu wanagundua kwamba uovu ndicho chanzo cha matatizo yote yanayomkabili mwanadamu. Wanadamu <u>Wameona madhara ya uovu, na matokeo yake ya kutisha, na sasa swali kubwa wanalojihoji ni kwamba yawezaje yote haya kutokea chini ya utawala wake Yeye aliye Mtakatifu, tena  aliye na uwezo na upendo mwingi?</u> Maswali mengine yanayoambatana na hoja hii ya msingi ni kama vile:

- Kwa nini kuna dhambi, maumivu na mateso?
- Ikiwa Mungu ni mwema kwa nini dunia inaonekana mbaya kiasi hiki?

Kwa nini Mungu hakuzuia dhambi isitokee kwa uwezo wake na akaiacha? Hapa

kuna fumbo kubwa ambalo wengi wetu hawajapata majibu bado, lakini somo hili litatoa majibu hayo kwa kadri ya nuru iliyofunuliwa kwetu katika maandiko matakatifu.

## MUNGU HAKUANZISHA PAMBANO HILI

Hakuna jambo lililofundishwa waziwazi katika maandko kuliko hili, kwamba: Mungu hakushiriki kwa namna yoyote ile katika ujio wa dhambi duniani;....

> Hakuna upungufu wowote uliojitokeza katika utawala wa Mungu uliopelekea kuibuka kwa dhambi. Dhambi ni mvamizi, ambaye uwepo wake hauwezi kupata sababu ya msingi. Ni fumbo, *ni kama kitendawili kisicho na jibu*; kuitafutia sababu ni kuitetea. Ikiwa sababu ya kuwepo kwake ingepatikana au kuonyweshwa, ingelikoma kuitwa dhambi tena. Maelezo tuliyonayo juu yake ni yale yanayopatikana katika maandiko matakatifu; ni "uasi wa sheria;" ni vita ya tamaa ya uvunjifu wa sheria dhidi ya kanuni ya upendo ambayo ni msingi wa utawala wa ufalme wa Mungu.

*{The Great Controversy 492.2}*

Ndiyo maana dhambi inaitwa "siri ya kuasi" katika 2 Wathesalonike 2:7. Sisi hatuwezi kwa sasa kuelewa kila kitu kuhusu pambano hili, isipokuwa, tunapewa mambo ya msingi ambayo yatatusaidia kutoka katika pambano hili tukiwa salama; na baada ya pambano hili, simulizi ya kisa hiki cha ukombozi na pambano lilivyokuwa itaendelea baada ya kukombolewa.

Cha kwanza kufahamu ni kwamba Mungu hakuhusika kwa namna yoyote ile kuanzisha pambano hili; Yeye anakuja kuingilia kati katika kuviondoa viumbe kwenye hatari zinazotokana na pambano hili na kisha anavisaidia viumbe kwa upendo, kuona hatari zilizomo ndani ya pambano ili viweze kuwa salama endapo viumbe hivyo vitachagua kuwa salama.

## MUASISI WA PAMBANO KUU

Biblia inaeleza wazi kabisa kwamba mwanzo wa kuwepo kwa uovu, ambao ndio umepelekea kuwepo kwa pambano lenyewe, ni kwa Ibilisi.

> atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo.
> 1 YOHANA 3:8

Hapa maandiko matakatifu yanaonyesha kwamba mwasisi na chanzo cha uovu ni Ibilisi na sio Mungu. Mara nyingi tunapopatwa na mambo mabaya huwa tunamlaumu Mungu na tunajaribiwa kulitukana jina lake, lakini ukweli kabisa ni kwamba, Ibilisi ndiye mwanzilishi wa uovu na madhara yake yote yanayojitokeza kwa namna mbalimbali. Kama ni lawama zilipaswa zimwendee Shetani sio Mungu.

Hili jina "Ibilisi" linatajwa mara 29 ndani ya Biblia ya Kiswahili, wakati jina "Shetani" (Ambalo ni jina jingine la Ibilisi) linatajwa mara 59. Katika kujifunza Biblia ni muhimu

sana kuzingatia kile ambacho Mungu anakitaja kwetu hata kama kimetajwa mara moja. Sasa kitu kinapotajwa zaidi ya mara moja, haifai kukipuuza. Biblia inataja majina kadhaa ya kiumbe hiki katika sehemu kadha wa kadha za Biblia. Haya ni baadhi ya majina yake baada ya kuasi kwake:

**Nyoka wa Zamani, Joka, Shetani (Ufu. 12:9–10), Ibilisi (Math. 4:10, 11), Beelzebuli (Math. 12:24), Beliali (2 Kor 6:15), Mjaribu (Math. 4:3), Adui (Math. 13:39, 13:25), Mshitaki (1 Pe 5:8), Baba wa Uongo (Yoh. 8:44). Mungu wa Ulimwengu huu (2 Kor 4:4).**

Mungu anahitaji tumuelewe vizuri huyu adui yetu kwa sababu huwezi kupambana katika vita yoyote ile mpaka kwanza umemfahamu adui yako vizuri, vinginevyo hautakuwa na uwezo wa kumshinda.

**Ni muhimu kufahamu kwamba Ibilisi sio nguvu flani, au aina flani ya kitu cha kufikirika, au mawazo mabaya aliyonayo mtu. Ibilisi ni kiumbe halisi na anawajibika kwa uovu wote, maumivu na mateso yalilojaa humu dunianieo hii.**

Pesa sio Shetani kama wengi wanavyodhani, Shetani sio mawazo mabaya kama wengi wanavyodhani, Shetani sio mtu flani muovu sana. Shetani ni kiumbe halisi ambacho asili yake sio hapa duniani. Tazama aya za Biblia zinavyosema kuhusu asili yake:

Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri (LUSIFA), ....
ISAYA 14:12

Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye....
UFUNUO 12:9

Biblia inasema asili yake ni mbinguni na alitupwa kutoka huko. Kwa hiyo basi, Shetani si kitu kingine cha kufikirika bali ni kiumbe halisi kabisa kilichokuwa mbinguni. Anawaweza kujigeuza gueza katika maumbile kadha wa kadha kama tutakavyoona hapo baadaye katika mwendelezo wa somo lakini mpaka hapa jambo la msingi kuelewa ni kwamba Shetani yupo na wala si kiumbe cha kufikirika.

## KUASI KWA LUSIFA

Mungu hakumuumba Ibilisi akiwa Ibilisi bali hapo mwanzoni alikuwa Malaika Mkamilifu.

Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako.
EZEKIELI 28:15

Mungu hakumuumba Shetani, bali alimuumba Lusifa. Alipoumbwa alikuwa kiumbe Mkamilifu. Maana ya neno mkamilifu ni:

1. Pasipo upungufu, enye ubora wa hali ya thamani sana
2. _enye kutokulaumika; bila hatia (kitabia)
3. _enye kutokuwa na mapungufu ya kimaumbile
4. _enye ukamilifu wa kitabia
5. enye ukamilifu wa kwa nyanja zote katika wakati wote

*James Swanson, Dictionary of Biblical Languages with Semantic Domains : Hebrew (Old Testament) (Oak Harbor: Logos Research Systems, Inc., 1997).*

Mungu angalimuumba Lusifa kama kikarakosi (robot), lakini vikarakosi haviwezi kuwa na upendo wala kufanya maamuzi ya kimaadili. Kwa hiyo tunaposoma kwamba alikuwa Mkamilifu, ni pamoja na hali ya kuwa na uwezo wa kufanya uchaguzi. Kama kiumbe kina akili lakini hakiwezi kufanya uchaguzi wake au hakina utashi, maana yake kiumbe hicho hakiko TIMAMU (SI KIKAMILIFU). Lusifa alikuwa timamu na hiyo inamaana alikuwa na uwezo wa kuchagua kumpenda na kumtii Mungu au kufanya vinginevyo. Tazama nabii alivyoonyeshwa jinsi alivyokuwa:

> Lusifa alipokuwa mbinguni, kabla ya uasi, alikuwa malaika wa cheo cha juu sana, heshima yake ilikuwa mara tu baada ya heshima ya Yesu. Uso wake, kama malaika wengine ulikuwa uso wa upole, na wakati wote alionyesha kuwa na furaha. Uwezo wake wa kiakili ulikuwa wa hali ya juu sana na uliopanuka mno, alionekana mwenye uwezo mkubwa sana wa kiintelijensia. Maumbile yake yalikuwa yenye hali ya ukamilifu; mwenendo wake ulikuwa bora sana na ulileta fahari kubwa. Alikuwa na nuru ya pekee iliyong'aa sana katika uso wake na kuzunguka umbo lake na alikuwa malaika mzuri kuliko malaika wengine wote;

*Ellen Gould White, The Story of Redemption (Review and Herald Publishing Association, 1947), 13.*

Kilimchomfanya kuasi ni tamaa ya kuinuliwa kuliko Yesu kwa sababu ya uzuri:

> 17 Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako; umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako; nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama.
> EZEKIELI 28:17

> Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini.
> ISAYA 14:13,14

> Kristo Mwana wa Mungu, tangu awali alikuwa na mamlaka juu ya majeshi yote ya mbinguni. Yeye na Baba walikuwa wamoja kabla ya kuumbwa kwa malaika. Lusifa alimuonea wivu Kristo, na taratibu alianza kuchukua mamlaka ambayo ilikuwa ya Kristo peke yake.

*Ellen Gould White, The Story of Redemption (Review and Herald Publishing Association, 1947), 13.*

Ukiendelea kusoma kitabu cha Kisa cha Ukombozi (The Story of Redemption, kuanzia ukurasa wa 13), kuna matukio yanayotajwa baada ya Lusifa kuanza kutamani nafasi ya Yesu:

- Lusifa aliendelea kusujudu mbele za Mungu japo moyoni hakuwa ameridhia
- Mungu aliita kikao cha malaika wote na akaelezea nafasi ya Yesu waziwazi
- Lusifa hakuridhika na maelezo ya Mungu na aliita kikao kingine cha malaika

Huku akificha makusudi yake, aliita mkutano wa malaika. Alileta agenda, ambayo ilimuhusu yeye mwenyewe. Kama aliyeumizwa, alihusianisha jinsi Mungu alivyompatia kipaumbele Yesu kama jambo lilimfanya yeye kuonekana amepuuzwa. Aliwaeleza kwamba utamu wa uhuru wote waliokuwao malaika ulikuwa sasa unaenda kufika mwisho wake. Je, kama wasingepewa kiongozi mwingine ni nani ambaye malaika wangempatia heshima yao? Aliwatamkia kwamba amewaita pamoja ili awahakikishie kwamba asingeweza kuvumilia tena huu uvamizi wa haki zake na haki zao pia; na kwamba yeye asingemsujudia tena Kristo; na kwamba atajitwalia heshima hii juu yake yeye mwenyewe ambayo alidai ilipaswa kuwa yake, na kwamba angekuwa kamanda wa wote ambao wangekubali kuwa chini yake na kuisikia sauti yake.

Palitokea mzozo miongoni mwa malaika. Lusifa na wafuasi wake walikuwa wanapambana kubadilisha ufalme wa Mungu. Hawakuwa wametosheka na hawakuwa na furaha maana walishindwa kuona makusudi ya hekima ya Mungu katika kumuinua Mwana Wake, na kumpatia uwezo usio na mipaka na amri isiyokuwa na mipaka pia. Waliamua kuasi dhidi ya mamlaka ya Mwana.

*Ellen Gould White, The Story of Redemption (Review and Herald Publishing Association, 1947), 14–15.*

Yohana wa Kisiwa cha Patmo na Paulo, waliliona pambano hili hivi:

**Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; ....**
UFUNUO 12:7

**Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, ....**
WAEFESO 6:12

Mapambano hayo yalikuwa juu ya:

1. Falme: Nani anastahili nafasi ya juu zaidi. Je, ni Shetani au ni Mungu. Je, viumbe vyenye utashi vinachagua kuwa upande gani: Upande wa Mungu au wa Shetani? Je, Yesu anastahili kuwa sawa na Mungu? Je, Yesu ni Mungu?
2. Mamlaka: Je, tutafuata kile ambacho Mungu anasema tufanye au tutafuata kile ambacho Shetani anaita uhuru wa kujiamulia mwenyewe? Je, tutakubali kutembea tukizingatia amri za Mungu au tunaamua kufanya kama tunavyotaka wenyewe? Je, tutafuata kanuni za maisha kama zilivyoletwa na Mungu au tutaziasi sheria zake?

Katika mapambano yaliyofanyika kule mbinguni, Lusifa hakushinda na hivyo alifukuzwa kutoka mbinguni.

nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni. 9 Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye.
UFUNUO 12:8, 9

Kwa nini Mungu hakumuangamiza Ibilisi na aliamua kumuacha? Kwa sababu Mungu hatumii mabavu, hapo mbele utaona pia kwamba ni kwa sababu uasi wa Shetani ulikuwa bado haujaeleweka vizuri kwa viumbe vingine.

Mungu angeweza kumuharibu Shetani pamoja na wale waliomuunga mkono kirahisi kabisa mithili ya mtu anayedondosha kipande cha jiwe chini; lakini hakufanya hivyo. Uasi haukupaswa kushindwa kwa mabavu. Mambo ya mabavu yanapatikana tu katika utawala wa Shetani. Kanuni za Bwana si za namna hiyo. Mamlaka yake yako juu ya wema, neema, na rehema; na hiyo ndiyo njia ambayo Mungu aliona itumike. Ufalme wa Mungu unazingatia maadili, na ukweli pamoja na pendo ambayo ni nguvu inayoshinda.

*Ellen Gould White, The Desire of Ages, vol. 3, Conflict of the Ages Series (Pacific Press Publishing Association, 1898), 759.*

Shetani alipata wafuasi ambao walifukuzwa pamoja naye, kwa hiyo hayuko peke yake.

Jeshi lote la mbinguni waliitwa mbele ya Baba ili kuamua kila hoja. Hapo ndipo ilipoamuliwa kwamba Shetani afukuzwe kutoka mbinguni, pamoja na malaika ambao waliungana naye katika uasi. Ndipo kulikuwa na vita mbinguni. Malaika walihusika pia katika vita; Shetani alitamani kumshinda Mwana wa Mungu na wote waliojisalimisha kwa mapenzi yake. Lakini malaika wazuri na waliosimama katika kweli walishinda, na Shetani, pamoja na wafuasi wake, waliondolewa mbinguni

*Ellen Gould White, Early Writings of Ellen G. White (Review and Herald Publishing Association, 1882), 146.*

Pia alipofukuzwa kutoka mbinguni mlango wake wa rehema ulifungwa maana Biblia inasema nafasi yake haikuonekana tena mbinguni.

## Mbinguni Alipofukuzwa Shetani ni Wapi?

1. Mbingu ni anga hewa (Atmosphere)

6 Mungu akasema, na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji. 7 Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo; 8 Mungu akaliita lile anga mbingu.
Mwanzo 1:6 - 8

### 2. Mbingu ni Anga Lenye Nyota

Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako, Mwezi na nyota ulizoziratibisha
Ayubu 8:3

### 3. Mbingu ni Makao Makuu ya Makazi ya Mungu

2 Namjua mtu mmoja katika Kristo, yapata sasa miaka kumi na minne, (kwamba alikuwa katika mwili sijui; kwamba alikuwa nje ya mwili sijui; Mungu ajua). Mtu huyo alinyakuliwa juu mpaka mbingu ya tatu. 3 Nami namjua mtu huyo, (kwamba alikuwa katika mwili sijui; kwamba alikuwa nje ya mwili sijui; Mungu ajua); 3 Nami namjua mtu huyo, (kwamba alikuwa katika mwili sijui; kwamba alikuwa nje ya mwili sijui; Mungu ajua); 4 ya kuwa alinyakuliwa mpaka Peponi, akasikia maneno yasiyotamkika, ambayo haijuzu mwanadamu ayanene.
2 Wakorintho 12:2-4

Baada ya Shetani na wafuasi wake kufukuzwa nje ya mbingu, walitamani kurudishwa tena mbinguni, lakini haikuwezekana maana hawakuwa na toba ya kweli.

Baada ya Shetani pamoja na wale walioanguka pamoja naye kufungiwa nje ya mbingu, na kugundua kwamba milele alikuwa amepoteza uzuri na utukufu wote wa mbingu, alitubu, na alitamani kurudishwa mbinguni. Alikuwa tayari kurudishwa katika nafasi yake ya awali, au kuchukua nafasi yoyote ile atakayopewa. Lakini hapana; ni lazima mbingu zisihatarishwe tena. Mbingu nzima ingeweza kuharibiwa kama angeweza kurudishwa tena; kwa kuwa dhambi ilianzia kwake, na mbegu za uasi zilikuwa ndani yake. Wote, yeye na wafuasi wake walilia, na wakasihi sana kurudishwa katika pendo la Mungu. Lakini dhambi yao -- chuki yao, wivu wao na tamaa yao--ilikuwa kubwa mno kiasi kwamba Mungu hakuweza kuiondoa kwao. Ililazimu sasa ibaki hivyo ili kupokea adhabu ya mwisho.

*Ellen Gould White, Early Writings of Ellen G. White (Review and Herald Publishing Association, 1882), 146.*

Shetani alipotupwa nje ya mbingu, aliruhusiwa kuyajaribu malimwengu mengine na hata sasa bado anaruhusiwa kufanya hivyo mpaka wakati wa mileniam atakapofungwa kifungo cha miaka elfu moja, ndipo hataruhusiwa kuyaendea malimwengu mengine. Alizuiliwa tu, kuingia mbinguni (mahali pa makao makuu ya Mungu).

Hapa [dunia ikiwa katika hali ya ukiwa] patakuwa nyumbani kwa Ibilisi kwa miaka elfu moja. Atakuwa amefungiwa, akizunguka-zunguka kwa kupanda na kushuka juu ya uso wa dunia ulioharibika ili aone madhara ya uasi wake dhidi ya sheria ya Mungu. Kwa miaka elfu moja atafurahia matunda ya laana aliyoisababisha. Akiwa amefungiwa katika ulimwengu huu, hatakuwa na nafasi tena ya kwenda katika sayari nyingine, na kuwajaribu au kuwachokoza wale ambao hawakuanguka.

*Ellen Gould White, Early Writings of Ellen G. White (Review and Herald Publishing Association, 1882), 146.*

Kando ya sayari hii dunia; Mungu ameumba sayari nyingine nyingi ambazo hazikuanguka dhambini. Ni nyingi kiasi kwamba hazihesabiki.

> Wanadamu wanaoishi katika haka ka-ulimwengu kadogo sana wanaukomo (wa kiakili); Mungu anayo malimwengu yasiyohesabika ambayo yanautii kwa sheria Zake na yanayoongozwa kwa kadri ya utukufu wake....

*Ellen Gould White, Counsels to Parents, Teachers, and Students Regarding Christian Education (Pacific Press Publishing Association, 1913), 66.*

Hapa Duniani, si mahali pekee palipokuwa na mti wa ujuzi wa Mema na Mabaya. Jaribu kama hilo hilo lilikuwepo pia mahali kwingine. Nabii alionyeshwa moja na sayari ambazo hazikuasi katika njozi na akauona mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

> Bwana amenipatia kuona malimwengu/sayari nyingine. Nilipewa mabawa, na malaika akaniongoza kutoka jijini kwenda mahali palipong'aa na kuwa na utukufu. Majani yake yalikuwa na kijani hai, na ndege walitoa sauti za wimbo mtamu. Wakazi wa mahali pale walikuwa na maumbile ya ukubwa wa namna tofauti tofauti; walikuwa wakamilifu, wenye fahari, na wenye upendo. Walikuwa na mwonekano wa sura ya Yesu, na nyuso zao ziling'aa kwa furaha ya utakatifu, zikionyesha uhuru na furaha waliyokuwanayo pale. Nilimuuliza mmoja wapo kwa nini walikuwa na upendo kuliko wale wa duniani. Jibu lilikuwa, "Tumeishi kwa utii mno kwa amri za Mungu, na hatukuanguka kwa kutokutii, kama wale walioko duniani." Kisha nikaona miti miwili, mmoja ulionekana kama mti wa uzima uliokuwa kule jijini. Matunda yote yalionekana mazuri, lakini matunda ya mti mmoja hawakupaswa kuyala. Walikuwa na uwezo wa kuyala yote, lakini walikatazwa kula ya mmoja. Kisha yule malaika aliyeniongoza akaniambia, "Hakuna mmoja wa hawa aliyeonja katika mti uliokatazwa; lakini kama wangekula, wangeanguka." Kisha nikapelekwa katika ulimwengu uliokuwa na mbalamwezi saba. Pale nilimuona Henoko mwema wa kale, aliyetwaliwa. Katika mkono wake wa kuume alishikilia tawi la mtende lililojaa utukufu na katika kila jani lake paliandikwa "Ushindi." ........ Nilimuuliza kama hapa ndipo alipoletwa baada ya kutwaliwa kutoka duniani. Alisema, "Hapana; kule jijini ndipo nyumbani, na hapa nimekuja tu kupatembelea." Alikuwa akitembea tembea mahali pale kana kwamba ni nyumbani kwake kabisa. Nilimuomba yule malaika aliyeniongoza angalau nibaki hapo kidogo. Sikuweza kuvumilia kuwa na wazo la kurudi tena kwenye hii dunia iliyo gizani. Kisha malaika akasema, "Imekupasa kurudi sasa, na kama utakuwa mwaminifu, wewe, pamoja na wale 144,000, mtapata fursa ya kutembelea malimwengu/sayari zote na kuiona kazi ya mkono wa Mungu."

*Ellen Gould White, Early Writings of Ellen G. White (Review and Herald Publishing Association, 1882), 39–40.*

Maelezo hayo yanatosha kukuonyesha kwamba, hii vita ilienea si tu katika dunia hii bali pia na katika malimwengu mengine ambayo Mungu aliyaumba. Sayari dunia tu, ndiyo iliyoanguka. Hii inatufundisha kuwa dhambi haina kisingizio chochote.

# WAHUSIKA KATIKA PAMBANO KUU

Katika pambano kuu kuna pande kuu mbili. Kuna viumbe wanaosimama upande wa Mungu na kisha kuna upande wa Ibilisi ambaye yeye mwenyewe ni kiumbe pamoja na viumbe wengine wote ambao hawakubali kusimama upande wa Mungu.

**Wahusika Wakuu wa Pambano**

1. Mungu Mwenyewe Anapambana Dhidi ya Ibilisi
   Shetani ni muhusika namba moja kwa sababu yeye ni mwanzilishi wa hili pambano. Mungu anaingia katika hili pambano kwa kusukumwa na upendo wake maana angeweza tu kuvimaliza viumbe vyote na akaumba upya lakini alivipenda viumbe vyake na analazimika kupambana ili asipoteze viumbe walioasi na wale ambao wanampenda.

> Kulikuwa na vita mbinguni; **Mikaeli** na malaika zake wakapigana na **yule joka**, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake....
> Ufunuo 12:7

2. Malaika Wabaya na Malaika wema

> Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli **na malaika zake** wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao **pamoja na malaika zake**....
> Ufunuo 12:7

3. Wanadamu Wanaoishi Duniani

> Kwa maana **kushindana kwetu sisi**, si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.
> Waefeso 6:12

Wakati dunia hii ilipoumbwa, Shetani alikuwa tayari ameumbwa; na hata wakati Adam na Hawa wakiumbwa na kuwekwa katika Bustani ya Eden, Shetani alikuwa amekwisha kuasi tayari. Na baada ya Shetani kufukuzwa mbinguni alikuja kuwajaribu Adam na hawa na aliwaangusha katika jaribu lake pale bustanini.

> Kabla ya anguko la Shetani, Baba alizungumza na Mwana kuhusu kumuumba Mwanadamu. Walikusudia kuiumba dunia hii, na kuumba wanyama pamoja na viumbe vingine vilivyo hai juu yake, na kumfanya mtu katika sura ya Mungu, ili akatawale kama mfalme juu ya kila kila chenye uhai ambacho Mungu angekiumba. Baada ya Shetani kujua kusudi hili la Mungu, alimuonea wivu Kristo, na wivu wake ulikuwa kwa sababu Baba hakumuuliza yeye kuhusu suala la uumbaji wa mwanadamu.

*Spiritual Gifts, vol. 3 (Seventh-day Adventist Publishing Association, 1858), 36.*

4. Viumbe Wengine Wanaoishi Sayari Nyingine
   Tumekwisha kuona na kusoma kisa cha Ellen G. White alivyoonyeshwa katika njozi habari za malimwengu mengine na jinsi alivyoona kwamba wao pia

walijaribiwa lakini walisimama imara. Hao viumbe wengine hatujui kama ni wanadamu au vipi lakini nabii aliona wanafanana na Yesu (kama mwanadamu alivyoumbwa katika mfano wa Mungu). Hao mpaka sasa wanaendelea kujaribiwa. Hapo awali waliamua kusimama imara upande wa Mungu japo hawakuwa wamepata ushindi vizuri, hawakuwa wamejua vizuri hili pambano na maana yake; lakini baada ya kifo cha Yesu pale msalabani udanganyifu wa Shetani ulikosa nguvu kwao na wakathibitika katika uchaguzi na maamuzi yao.

Mbingu nzima na malimwengu ambayo hayakuanguka walikuwa mashahidi wa pambano. Kwa usikivu na mvuto mkubwa kabisa walifuatilia onyesho hili lililokuwa linaelekea katika miisho ya pambano. Walimtazama Mwokozi akiingia katika bustani ya Gethsemane, Roho yake iliinama chini kwa utisho wa giza kuu.

*Ellen Gould White, The Desire of Ages, vol. 3, Conflict of the Ages Series (Pacific Press Publishing Association, 1898), 759.*

**Hii ni sababu nyingine tena inayoonyesha kwa nini Mungu hakumuangamiza Ibilisi mara moja na kwa haraka.**

Kwa malaika na kwa malimwengu ambayo hayakuanguka kilio cha, "imekwisha," kilikuwa na maana kubwa sana. Ilikuwa kwa ajili yao na kwa ajili yetu pia kazi kubwa ya ukombozi ilikuwa imekamilishwa. Wao pamoja nasi wanashiriki matunda ya ushindi wa Yesu. Ni mpaka Kristo alipokufa msalabani ndipo tabia ya Shetani ilifunuliwa waziwazi kwa malaika na kwa malimwengu ambayo hayakuanguka. Mkuu wa uasi alikuwa amejivika udanganyifu kiasi kwamba hata viumbe watakatifu hawakuwa wameelewa ukweli *[kuhusu uasi]* wake. Hawakuwa wameona vizuri asili ya uasi wake.

*Ellen Gould White, The Desire of Ages, vol. 3, Conflict of the Ages Series (Pacific Press Publishing Association, 1898), 758.*

Shetani aliona kwamba kificho chake kilikuwa kimeondolewa. Uongozi wake ulikuwa umewekwa wazi mbele ya malaika ambao hawakuanguka na malimwengu yote. Alikuwa amejifunua kama muuaji. Kwa kumwaga damu ya Mwana wa Mungu, alikuwa amejing'oa kutoka katika kuhurumiwa na viumbe wa mbinguni. Tangu hapo kazi yake ilipata kikwazo. Hata awaze namna gani, asingeweza tena kuendelea kuwasubiri malaika wanaotoka katika mahakama za mbinguni, na mbele yao kuwashtaki ndugu wa Kristo kwamba wamevikwa mavazi ya giza na uchafu wa dhambi. Kiungo cha mwisho cha Shetani (kuhurumiwa na viumbe wa mbinguni) kilikuwa kimevunjwa.

*Ellen Gould White, The Desire of Ages, vol. 3, Conflict of the Ages Series (Pacific Press Publishing Association, 1898), 761.*

Hiyo inaonyesha waziwazi jinsi Mungu anavyotumia upendo na neema kuushinda uovu na ubaya na kufunua uongo ambao Shetani alikuwa ameusambaza kwa malaika. Shetani alidai kwamba Mungu ni dikteta na kwamba hana upendo kwa

viumbe vyake na kwamba sheria zake ni ngumu kiasi kwamba hakuna awezaye kuzitimiza, lakini maisha ya Yesu na kifo chake msalabani kilimdhihirisha Ibilisi na nia yake. Hii ndiyo sababu Mungu hakumuangamiza haraka Ibilisi ili viumbe wote wajifunze kwa kuona wenyewe. Kama angemuangamiza mapema viumbe wangemuogopa Mungu badala ya kumpenda, lakini sasa mpaka hapo, viumbe vyote vilijiridhisha na ukweli usiopingika kwamba Mungu ni Pendo.

## MBINU ZINAZOTUMIKA KATIKA PAMBANO KUU

Ukweli ni kwamba, wote tuliomo duniani tayari tumeshaingia katika Pambano Kuu. Kama tulivyosoma (rej. Waefeso 6:12), sisi tayari tumo ndani ya mapambano haya maana Biblia inasema "Kwa maana kupigana kweti sisi...;" Hii inatosha kumjulisha kila mtu kwamba wanadamu tumo ndani ya Pambano. Hili pambano (rej. Waefeso 6:12) ni "juu ya falme" na "juu ya mamlaka." Hapa tunamambo makubwa mawili ambayo juu yake, Pambano lote hili linajengwa.

### Katika Suala la Falme

Kwa lolote tunalolifanya tunaonyesha kuutambua Ufalme wa Mungu kwetu yaani kuonyesha kwamba tunamkubali Mungu kama mtawala na mwenye mamlaka juu yetu na ya kwamba Yeye ni Mungu na sisi ni viumbe vyake; au tunaonyesha kutokumtambua na kudai kwamba Yeye si Mungu kwetu. Hapa anachofanya Ibilisi ni kujaribu kuviondolea viumbe uchaji Mungu. Upotoshaji wa awali kabisa uligusa kuipinga Nafsi ya Pili ya Mungu yaani Mungu Mwana. Kwa kufanya hivyo alimgusa Mungu moja kwa moja (Nafsi ya Mungu Baba na Mwana hazijawahi kutenganishwa).

> yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, ...
> 2 Wakorintho 5:19

Shetani alitafuta kuiharibu Ibada ambayo ni mahusiano ya Mungu na viumbe vyake pamoja na heshima ya viumbe kwa Mungu muumbaji. Neno linatukumbusha haya:

> akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.
> Ufunuo wa Yohana 14:7

### Katika Suala la Mamlaka

Katika lolote tunalolifanya tunapaswa kuonyesha kwamba tunamheshimu Mungu na katika hili kipimo ni kufanya yale anayosema tufanye, kisha kuacha yale anayosema tuyaache. Kukiuka maagizo yake ni kuingia katika mtego wa Shetani na kukubaliana naye kwamba yale madai yake ya kuvitaka viumbe visimtii Mungu wala kufuata kanuni au sheria ua maagizo yake, lilikuwa jambo sahihi. Ukweli ni kwamba yule tunayemtii, ndiye tunayemuunga mkono na kwa namna hiyo tunafanyika watumwa wake. Hii ni ushahidi kwamba hakuna asiye na uchaguzi:

> Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki.
> Warumi 6:16

### Silaha Kubwa za Ibilisi

Shetani anatumia silaha kubwa mbili. Silaha ya kwanza ni uongo na silaha ya pili ni mabavu. Katika uongo lengo lake ni kupotosha ukweli kuhusu Mungu, Tabia yake, Sheria yake na maagizo yake ili viumbe visielewe ukweli kuhusu Mungu alivyo na dhamira yake kwa viumbe wake. Hiyo ni njia inayotumia ushawishi; hapa anajitahidi kadri anavyoweza ili kuuharibu mtazamo wa mtu kuhusu Mungu. Silaha ya pili anayotumia ni mabavu: hapa anatesa, anatishia na hata wakati mwingine anaua ili kuvilazimisha viumbe kumkataa Mungu au kupoteza mahusiano na Mungu kwa kuogopa kuingia katika hatari. Anaweza kuanza na silaha yoyote kukushambulia:

> Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi, na tamaa za baba yenu ndizo mpendazo kuzitenda. Yeye alikuwa **mwuaji tangu mwanzo**; wala **hakusimama katika kweli**, kwa kuwa hamna hiyo kweli ndani yake. Asemapo uongo, husema yaliyo yake mwenyewe; kwa sababu **yeye ni mwongo**, na baba wa huo.
> YOHANA 8:44

Lakini silaha zake zote hizo mbili hazina haja ya kuwatisha watu wa Mungu kwa sababu wakati wote watu wa Mungu wako na ulinzi kutoka mbinguni. Mungu wetu ni mkuu kuliko Shetani na Yeye yuko ndani yetu; Pia amewapatia wanadamu ulinzi wa Malaika ambao kazi yao ni kuwalinda wanadamu na kuwaokoa katika hatari.

> Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu nanyi mmewashinda, kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.
> 1 Yohana 4:4

> Malaika wa BWANA hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa.
> Zaburi 34:7

### Mbinu Anazotumia Shetani Katika Pambano

Shetani anazo akili nyingi tu, kama tulivyoona jinsi alivyoumbwa. Kwa hiyo anapokuja kumjaribu mtu haji akijitambulisha kwamba Yeye ni Shetani. Anajificha nyuma ya udanganyifu flani ambao kwa haraka-haraka unaonekana kuwa ni kama kitu cha kupendeza. Huwa anatabia ya kuigiza-igiza mambo yanayotaka kufanana na mambo ya mbinguni, lakini wale wanaosoma maandiko watamgundua na watakuwa salama. Hebu tazama mifano hii michache ambayo inaonyesha jinsi Shetani anavyojaribu kuigiza igiza mambo mazuri. Shetani anauwezo wa kuigiza mwonekano wa Malaika. Hii ni tahadhari kwamba katika kupambana naye tusitegemee macho yetu au fikra zetu kutokana na kile tunachoona, bali neno.

> Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru.
> 2 WAKORINTHO 11:14

Shetani anauwezo wa kuigiza Mwonekano, japo si kwa asilimia 100%. Ndiyo maana Yesu alisema mkisikia yuko mahali flani msitoke wala msiamini. Hapa mkazo ni ule ule kwamba tusitembee kwa kuona na kushawishika kwa macho, tutembee kwa neno la Mungu, ndipo tutakuwa salama.

Wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule msisadiki. Mathayo 24:23

Kielelezo cha kumshinda Shetani tunakipata kwa Yesu mwenyewe. Alipojaribiwa na yule mwovu alimshinda kwa kumwambia "imeandikwa" (Luka 4:4, 8, 16). Kupitia Neno la Mungu tutapata kujua mbinu za kumpinga, kuepuka majaribu yake na hata kustahimili vitisho vyake na hatimaye kumshinda. Zifuatazo ni mbinu anazozitumia Shetani katika Pambano Kuu:

### *01: Ananukuu Vibaya Maandiko ili Adanganye na Kupotosha Maana Kusudiwa*

Mathayo 4:5, 6 akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa, **Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe**.

Zabiri 91:11 **Kwa kuwa atakuagizia malaika zake Wakulinde katika njia zako zote. Mikononi mwao watakuchukua, Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.**

Katika sehemu hii ya maandiko alinukuu baadhi ya maneno kama yalivyo lakini pia alipunguza baadhi ya maneno. Ukilinganisha vizuri hizo aya utagundua kwamba alivyofoa maneno "Wakulinde katika njia zako zote." Wale wasiosoma maandiko na kuyachunguza kwa umakini wako katika hatari ya kupotoshwa na Shetani. Mbinu hii ndiyo iliyotumika pia kuwaangusha Adam na Hawa na hivyo kumpatia Shetani nafasi hapa duniani. Wakati mwingine Shetani anachukua maneno ya Mungu na anayageuza kidogo; Usalama wetu ni kufuata maagizo ya Mungu kama yalivyotolewa na hatupaswi kuyaongeza au kuyapunguza. Tazama kwa makini kile alichosema Mungu na kile anachosema Shetani.

Mwanzo 2:16 BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, **Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula**, 17 **walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile**, kwa maana siku **utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika**.

Mwanzo 3:1 Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, **Msile matunda ya miti yote ya bustani?** 4 Nyoka akamwambia mwanamke, **Hakika hamtakufa**,

### *02: Anawatesa Watu wa Mungu ili Waiache Imani yako*

Shetani anatumia njia za mateso. Mateso yanaweza kuja kwa kupigwa, kutupwa gerezani, kunyanyaswa, kuonewa, kufanya maisha yawe magumu, kupoteza mali, kukushushia heshima na mambo mengine mengi yanayomfanya mtu akose raha ya maisha ya dunia hii. Mtu anapokubali kuvunja maagizo ya Mungu au anapomkana Mungu ili apate ahueni, kwa mtazamo wa haraka inaonekana anakuwa anatafuta nafuu ya maisha lakini ukweli ni kwamba maamuzi kama hayo ni lugha nyingine ya kumkana Mungu na kumpatia Shetani ushindi. Tunapaswa kujua kwamba Shetani ataleta majaribu lakini tunapaswa kujua pia imetupasa kusimama imara hata kama wakati mwingine imetupasa kupoteza mambo ya ulimwengu huu.

Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari....
Ufunuo 12:13

Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. **Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima**.
Ufunuo wa Yohana 2:10

Biblia imejaa ahadi za Mungu nyingi zinazoonyesha kuwa Yeye yuko pamoja na sisi wakati wote na atatupigania. Pamoja na yote hayo inatupasa kujua kwamba hata kama tunafahamu kuwa anao uwezo kutuokoa bado tunapaswa kuwa waaminifu hata katika nyakati atakazoamua kuacha tupoteze ikibidi hata uhai. Kupoteza uhai sio mwisho wa Maisha, siku moja waaminifu wa Mungu watafufuliwa na maisha yataelndelea.

Kwa hiyo hatulegei; bali ijapokuwa utu wetu wa nje unachakaa, lakini utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. 17 **Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana**; 18 tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele.
2 Wakorintho 4:16, 18

## *03: Hutenda Miujiza ili Kuwadanganya Yumkini Hata Wateule*

**Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara**, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.
Ufunuo wa Yohana 16:14

Kadri tunavyoelekea mwisho wa wakati, Shetani atafanya miujiza mingi sana akijificha nyuma ya jina la Ukristo ili awapotoshe wengi. Ni wasomaji tu wa neno, na wale wanaojivika silaha zote za vita (Waefeso 6:12), ndio wataweza kusimama. Hebu tazama baadhi ya mambo machache ambayo Shetani atayafanya kwa lengo la kuwapotosha wateule wa Mungu.

> Kuna mambo ya ajabu, ambayo yatakuwa yameunganika na shetani kwa karibu kabisa, yatatokea hivi karibuni. Neno la Mungu linasema kwamba Shetani atafanya miujiza. Atawafanya watu kuugua, na kisha kwa haraka ataondoa uwezo wake wa kishetani. Hao wataonekana kama wamepokea uponyaji. Hizi kazi hatimaye zitawaleta Waadventista wa Sabato wengi katika kipimo.
> --- Selected Messages 2:53 (1904). --- Last Day Events 166.4

> Atafanya hili la kumuigiza Kristo. Atajivika mwenyewe mavazi ya kifalme ambayo yameelezwa kwa usahihi na njozi ya Yohana. Anao uwezo wa kufanya hivyo.
> --- Last Day Events 164.1

Namna Kristo alivyofanya kazi ilikuwa kwa kulihubiri neno, and to relieve suffering by miraculous works of healing. But I am instructed that we cannot now work in this way, [Miracles will accompany the ministry of God's people under the loud cry (see Chapter 14), but they will not have the significance they did in Christ's day. The performing of miracles will no longer be a proof of divine endorsement.] for Satan will exercise his power by working miracles. God's servants today could not work by means of miracles, because spurious works of healing, claiming to be divine, will be wrought.—Selected Messages 2:54 (1904). LDE 169.2

Yesu alituonya katika neno lake akitutahadharisha na mambo haya yanayoujia na ambayo tayari yameshaanza kuupata ulimwengu huu.

Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule. 25 Tazama, nimekwisha kuwaonya mbele. 26 Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki.
Mathayo 24:24 - 26

## *04: Anatumia Wachungaji wa uongo na anawapatia uwezo*

13 Maana watu kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo. 14 Wala si ajabu. Maana Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru. 15 Basi si neno kubwa watumishi wake nao wakijigeuza wawe mfano wa watumishi wa haki, ambao mwisho wao utakuwa sawasawa na kazi zao.
2 Wakorintho11:14 - 15

Biblia inatuelekeza kutokuamini kila roho bali kuzijaribu hizo roho.

Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.
1 Yohana 4:1

## *05: Analeta Maumivu na Magonjwa ili Mtu Atende Dhambi*

Basi Shetani akatoka mbele za uso wa Bwana, akampiga Ayubu na majipu mabaya tangu wayo wa mguu hata utosi wa kichwa. 9 Ndipo mkewe akamwambia, Je! Wewe hata sasa washikamana na utimilifu wako? Umkufuru Mungu, ukafe. …Je! Tupate mema mkononi mwa Mungu, nasi tusipate na mabaya? Katika mambo hayo yote Ayubu hakufanya dhambi kwa midomo yake.
Ayubu 2:7,9

## *06: Anawafanya Watu Watawaliwe na Mapepo ili Awatawale Kabisa*

Pepo mchafu, amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika, asipate. 44 Halafu husema, Nitarudi nyumbani kwangu nilikotoka; hata akija, aiona tupu, imefagiwa, na kupambwa. 45 Mara huenda, akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza. Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi hiki kilicho kibaya.
Mathayo 12:43

Njia ya kumuondoa Shetani na kumnyima nafasi ya kutawala maisha yetu kupitia pepo wabaya ni kumtii Mungu na kumpinga Shetani. Ukiilea dhambi unampatia Shetani nafasi; usipomtii Mungu, unampatia Shetani nafasi ya kukutawala

Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.
Yakobo 4:7

## *07: Shetani Anatumia Mitego Mbalimbali ili Kuwaangusha Watu*

wapate tena fahamu zao, na kutoka katika mtego wa Ibilisi, ambao hao wametegwa naye, hata kuyafanya mapenzi yake.
2 Timotheo 2:26

Mtego ni kitu ambacho kwa nje kinaonekana ni kitu salama, lakini ukikichunguza kina hila inayoonyesha kuwa njia ya kukufanya usiwe mtii kwa Mungu, au usimpende au uhararibu mahusiano yako na Mungu. Katika muktadha huo, Shetani anaweza kutumia mtu, kitu, hali au mazingira flani ambayo yatakuongoza kutenda dhambi. La muhimu ni kuchunga mawazo, maamuzi na matendo yetu yasiende wala yasituongoze katika kutokumtii Mungu au katika kuvunja mahusiano naye.

**Mbinu anazotumia Mungu Katika Pambano**
Ili kuwaokoa watoto wake, Mungu anatumia neno lake kuwaongoza na kuwaandaa watu kufaa kuhusiana naye na kufaa kutenda matendo mema kwa ukamilifu. Hapa tunazungumzia neno lililoandikwa ambalo linatupatia siri za ushindi (Waefeso 6:11) na Neno aliyefanyika mwili na akafa msalabani kwa ajili ya ushindi wetu.

Waebrania 4:12 Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

Yohana 3:16 Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Wewe ambaye umepokea ujumbe huu, inakupasa ukae chonjo maana uko katika Pambano. Shetani anatamani akuangamize lakini Mungu anatamani akuokoe. Mungu ametutendea wema, ametuonyesha neema na rehema zake ili tusiweze kupotea milele; hayo ameyafanya kwetu kupitia kifo cha Yesu pale msalabani. Mungu anatualika kuchagua kuwa upande wa Ufalme wa Wake unaozingatia maadili, kweli pamoja na pendo ambavyo vina nguvu itakayotupatia Ushindi dhidi ya Ibilisi.  Mwishoni mwa haya mapambano, Mungu ataukomesha uovu na wala uovu hautatokea tena (Nahumu 1:9). Ni heri kuchagua kusimama upande wa Mungu hata kama wakati mwingine inaonekana kukugharimu kwa sababu baada ya kusimama upande wa Mungu katika maisha haya, hatimaye utaishi milele ukiwa na furaha na amani isiyokoma pamoja na Mungu (Ufu. 21:3)

